... ya Fedha na Mipango, Dkt. Charles Mwamwaja (katikati) akimkabidhi Naibu ... Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo tuzo ya mshindi wa jumla utunzaji bora wa hesabu kwa taasisi za umma. Bodi ya Uhasibu NBAA ndiyo waandaaji tuzo hizo. Makabidhiano hayo yalifanyika Jijini Dar es Salaam juzi. Wengine wanaoshuhudia ni viongozi wa TRA. (Picha na Prona Mumwi)

MAJIRA UK 10.

# Taasisi yapanga kutoa kwa akinamama wafugaji

**Na George Mwigulu, Katavi**

TAASISI ya Kawodeo inayojishughulisha na utunzaji wa mazingira na msaada wa kisheria katika Mkoa wa Katavi, imepanga kutoa elimu kwa akinamama wafugaji wa mifugo ili wajue haki yao ili waweze kuondokana na changamoto hiyo.

Hayo yalisemwa hapo jana na Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Fujensiana Kapama wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya utendaji kazi unaofanywa na taasisi hiyo.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa akinamama jamii ya wafugaji wengi kutojua haki zao za msingi za kibinadamu kutokana na uelewa mdogo wa kujua haki zao.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kutambua hilo, taasisi hiyo imepanga kuzunguka kwenye maeneo yote ya Mkoa wa Katavi kwa lengo la kutoa elimu kwa akinamama hao ili waweze kuelewa haki zao.

Veronica alisema watoto wengi ambao wamekuwa wakipewa mimba wakiwa na umri mdogo ni watoto wa wafugaji na wamekuwa hawajui hata kama watoto wao wamepewa mimba wapeleke wapi malalamiko yao ili hatua zichukuliwe.

Alifafanua kuwa wanawake wafugaji wamekuwa wakihamishwa na waume zao kutoka maeneo ya mikoa mingine kwenda kwenye mikoa mingine kama wao ni mizigo bila kutaka.

Mkurugenzi huyo alisema akinamama hao wamekuwa wanapelekwa kwenye maeneo ambayo hayana maji na wamekuwa wakilazimika kutembea umbali wa kilomita nne, kupata huduma ya maji na yote hiyo imekuwa ikitokana na kutojua haki zao za msingi.

Alisema wamekuwa wakifanya hamasa kwa wanawake na makundi ya pembezoni katika kusimamia na kufanya maamuzi juu ya rasrimali.

Naye Maria Kaboza ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitoleni Kata ya Stalike Halmashauri ya Nsimbo alisema siku za nyuma, wanawake walikuwa wakinyanyasika lakini hivi sasa wanamiliki mali kutokana na kazi, ambayo imefanywa na taasisi hiyo kwa kutoa elimu kwa wanawake.

Alisema kulikuwa na mila potofu, ambazo zilikuwa mwanamke hazitambui kuwa hawezi kumiliki mali kama ardhi, lakini kutokana na elimu hivi sasa wanamiliki ardhi.

Scanned with CamScanner

kuwa na wafanyakazi wenye sifa za kitaaluma katika tasnia hiyo.

mbili yaliyoanza Ijumaa.

"Kuingia kwa Benki ya NMB

lilikuwa ni kusaidia kuleta huduma za

wowote na hivyo kutoa kabisa changamoto ya umbali katika

MAJIRA UK 16.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel akionesha kuvutiwa na moja ya bidhaa inayozalishwa na wajasiriamali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alipotembelea banda la chuo hicho katika Maonesho ya Bidhaa za Viwanda yanayofanyika Viwanja vya Maonesho vya Mwalimu Nyerere (Sabasaba) Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

## ari Watanzania watano

ia
uli

imepiga
nbinu ya
sha elimu

kuwa na
ambao ni
vanjisi na
ari maelfu
makubwa
iaka 59 ya

ya tano
Tanzania
eza kuwa,
va bidii na
o.

ajiri

baye hakuwa
ikuu. Alikuwa
nye familia ya
ipoteza muda
a wasomi wa
nu za kujiajiri,
kufanya kazi
i mfano wake
e mabilionea,"

geza uongozi
mpango wao
a kozi mpya
nivu (PHD) na
nazingira bora
a ya Ngurdoto,
vanafunzi wa
kuja kusoma
lini.

cha Uhasibu
nan Sedoyeka,
ni miongoni
atika bara la
wanajipanga
Shahada za
ribuni.

# Serikali yawaonya wafanyabiashara wanaoongeza unga kwenye maziwa

**NA MWANDISHI WETU**

SERIKALI imewaonya baadhi ya wafugaji wenye mtindo wa kuongeza unga katika maziwa, kuacha kufanya hivyo kwa kuwa wanaharibu biashara ya maziwa katika soko la ndani ya nchina hata nje.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel, alitoa onyo hilo jana, alipotembelea banda la Maonesho la Bodi ya Maziwa, lililopo katika Viwanja vya Maonesho ya Bidhaa za Viwanda, yanayoendelea kufanyika katika Viwanja vya Maonesho vya Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Profesa Gabriel, alisema wanaofanya hivyo, wanapaswa kutambua kuwa kitendo hicho ni kibaya, wanajidanganya wenyewe na wasipojirekebisha wataishia pabaya.

"Bodi endeleeni kutafuna wale wote ambao wanachakachua maziwa kadri iwezekanavyo, sheria ichukue mkondo wake na hatutakuwa na huruma yeyote kwa sababu wanaharibu taswira nzima ya biashara ya maziwa ndani na nje ya nchi," alisema Profesa Gabriel.

Alisema wafugaji wanapaswa kutambua kwamba, serikali ina vipimo, ambavyo vinaweza kutambua maziwa yaliyowekwa unga, hivyo aliwataka wale wote wanaojihusisha na uhalifu huo, kuacha kufanya hivyo kwa kuwa watakaokutwa sheria itachukua mkondo wake.

Aidha, Profesa Gabriel, aliitaka Bodi ya Maziwa, kuhakikisha unywaji wa maziwa unaongezeka na wawahamasishe Watanzania kadri iwezekanavyo walau ndani ya miaka mitano ijayo, wazidi walau lita zaidi ya 100 kwa mwaka.

"Kwa sasa unywaji upo kwenye lita 54, jambo ambalo ni aibu kwa nchi yenye ng'ombe milioni 33.4 na inazalisha lita za maziwa bilioni 3.01, huku kukiwa na viwanda vya kuchakata maziwa 99.

"Bodi fanyeni kazi ya ziada, msifanye kazi kwa mazoea, wekeni sayansi kwenye kazi yenu na pia pimeni elimu mliyoitoa imeeleweka kiasi gani ili wale wanaofanya vizuri muwapongeze na wale wanaokosea, muwaadhibu kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kuifanya tasnia iwe bora zaidi," alisema.

Alisema anaamini tasnia hiyo ya maziwa itaendelea kusimamiwa vizuri na itachangia vizuri katika uchumi wa kati, ambao Rais Dk. John Magufuli, ameshafanya kazi ya ziada kuipeleka nchi katika uchumi wa kati miaka mitano kabla, hivyo anaamini nchi itaendelea kupanda kiuchumi na zao la maziwa ni muhimu likaendelea kuimarishwa ili litoe mchango unaohitajika katika kukuza pato la taifa.

"Bodi ya Maziwa hakikisheni ubora wa maziwa unakuwepo na yapatikane kwa wingi, kwa ajili ya kujenga afya bora kwa watumiaji," alisisitiza.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, alisema katika wilaya hiyo na Mkoa wa Dar es Salaam, watahakikisha wanaendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa kupitia michezo mbalimbali na wamejipanga hivi karibuni, wanatarajia kufanya tamasha kubwa, litalotumika kuchagiza pia unywaji wa maziwa nchini.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Noely Byamungu, alisema wamejipanga kuhakikisha wanajenga utamaduni kwa jamii kupenda kunywa maziwa na wameanza na kundi la wanamichezo, lakini kuna mpango mkakati wa kitaifa wa kuwafikia watoto mashuleni.

Scanned with CamScanner